


HAKI

# DC Kibaha kuunda kamati itakayotatua migogoro ya wakulima na wafugaji

Sanjito Msafiri, Mwananchi
smsafiri@mwananchi.co.tz

**Kibaha.** Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, Sara Msafiri amepiga marufuku kesi zinazohusisha masuala ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji kupelekwa wilayani na mahakamani, badala yake zishughulikiwe kwa ngazi ya vijiji husika.

Alisema kutakuwa na kamati maalumu itakayopewa mwongozo wa kuamua kesi hizo ili haki ipatikane kwa wakati na si kuonea mwingine.

Mkuu huyo wa wilaya amechukua hatua hiyo baada ya kuwapo malalamiko ya ucheleweshaji wa haki kwa mashauri yanayohusisha migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji wilayani humo.

Wakizungumza katika mkutano aliouitisha kwa ajili ya kuzikiliza kero mbalimbali za wakazi wa Kijiji cha Kimala Misale mkoani hapa, idadi kubwa ya watu waliotoa kero ni jamii ya wakulima waliodai asilimia kubwa ya mashauri ambayo chanzo chake ni wafugaji kulisha mifugo kwenye mashamba yao yamekuwa hayaishi kwa haki.

"Mfugaji analisha mifugo kwenye shamba, unapeleka malalamiko yako ofisi ya kijiji kwa ajili ya kulipwa fidia, lakini kiasi unachoambiwa ulipwe ni kidogo ukilinganisha na gharama ulizozitumia, hivyo ni hatari na ukikataa shauri likipelekwa mbele huko ndio kabisa, kesi itapigwa danadana hadi unakata tamaa na haki zote zinapotea," alisema Joseph Kuya, mmoja wa wakulima wa kijiji hicho.

Kwa upande wake mkulima wa kijiji hicho, Ally Selemani alisema kinachosikitisha ni kuwa inapotokea mfugaji amelisha kwenye shamba la mkulima fidia anayopangiwa ni ndogo, hivyo kufuatia maagizo ya mkuu wa wilaya kuwe uwekwe mwongozo wa malipo ya fidia kulingana na hali ya soko la wakati huo huenda itawasaidia.

"Tumeumia sana, unalima kwa gharama kisha wanakuja kulishwa wanyama na fidia unayopewa haieleweki," alisema Ally.



Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri (kulia) akisisitiza jambo alipokuwa akijibu kero mbalimbali za wakazi wa Kijiji cha Kimala Misale mkoani Pwani, jana. **Picha na Sanjito Msafiri**

**KERO**

**"Mfugaji analisha mifugo kwenye shamba, unapeleka malalamiko yako ofisi ya kijiji kwa ajili ya kulipwa fidia, lakini kiasi unachoambiwa ulipwe ni kidogo ukilinganisha na gharama ambazo umezitumia, hivyo ni hatari na ukikataa shauri likapelekwa mbele huko ndio kabisa, kesi itapigwa danadana hadi unakata tamaa na haki zote zinapotea," alisema Joseph Kuya.**

**Ally Selemani pia alilalamikia malipo anayokadiriwa kulipa mtu akilisha mifugo, hivyo kauli ya mkuu wa wilaya inaweza kuwasaidia kumaliza changamoto hiyo.**

# Ofisa Mtendaji atuhumiwa kwa utoro kazini

Hamida Shariff, Mwananchi
hshariff@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Wananchi wa kijiji cha Kododo Kata ya Luale Wilaya ya Mvomero wamemuomba Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kumchukulia hatua za kinidhamu Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Evarist King'ungwi kwa kile wanachodai kuwa ni mtoro kazini na kushindwa kusimamia miradi ya Serikali.

Akizungumza na *Mwananchi* juzi, Diwani wa Kata ya Luale, Jackson Msumi alisema kuwa mtendaji huyo wa kijiji amekuwa mtoro kazini na hivyo kushindwa kuwahudumia wananchi kwa wakati, kusimamia miradi inayoibuliwa na Serikali na ya wananchi, ukiwemo wa maji wa kijiji cha Kododo.

"Malalamiko ya wananchi ni ya kweli, huyu mtendaji amekuwa hana mahudhurio mazuri na anapoulizwa anadai anaumwa miguu, taarifa za vitendo hivyo zipo kwa mtendaji wa kata na hata kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, hivyo tunasubiri mrejesho kutoka huko," alisema Msumi.

Hata hivyo, King'ungwi alifafanua tuhuma za matumizi ya fedha za wananchi kwa kusema kuwa baada ya kuchangisha fedha zilibadilishiwa matumizi na kuamuliwa ziende kwenye ujenzi wa vyoo, lakini alizirudisha fedha hizo zipatazo Sh300,000 kwa Ofisa Mtendaji Kata kwa ajili ya utaratibu mwingine.

"Baadhi ya watu wanapanga kunidhuru, nilishatoa taarifa za maandishi kwa mkurugenzi na Kituo cha Polisi Mgeta, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa," alisema King'ungwi.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Amadei Mahita alisema kuwa mtendaji huyo amekuwa akimpa taarifa za kuumwa kwa njia ya simu na si maandishi.

"Kukosekana kwake ofisini mara kwa mara kunasababisha wananchi kukosa msukumo wa kuchangia miradi ya maendeleo," alisema Mahita.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash alikiri kupokea malalamiko hayo na uchunguzi unaendelea, ukivihusisha vyombo vingine, ikiwamo Mamlaka ya kuzuia na kupambana na Rushwa (Takukuru) na Jeshi la Polisi.

**'Nakiri kutokuwa na mahudhurio mazuri kwa sababu ninasumbuliwa na miguu, nilipata ajali ya pikipiki mara mbili mwishoni mwa mwaka jana, pia naogopa vitisho kutoka kwa wanaonichukia, kwani wameshanivamia mara mbili na kunipiga wakati natoka kazini.'**
Evarist King'ungwi

## Kwa Ufupi

### Watakiwa kuondoa urasimu uwekezaji sekta ya madini

**Morogoro.** Waziri wa Madini, Dk Dotto Biteko amewaagiza maofisa madini wakazi wa mikoa kuondoa urasimu kwa wawekezaji wanaoonyesha nia ya kuwekeza kwenye uchimbaji na biashara ya madini nchini Tanzania.

Waziri Biteko alitoa agizo hilo mjini Morogoro, kwenye kikao na viongozi wa Tume ya Madini, wakurugenzi na maofisa madini wakazi wa mikoa 29 ya kimadini. Alisema kuwa wawekezaji wengi kutoka nje ya nchi, hasa nchi jirani wameonyesha nia ya kutaka kuwekeza kwenye shughuli za madini, hivyo watendaji hao kuhakikisha wanafanya biashara badala ya kuwawekea vikwazo.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela alisema utendaji wenye ufanisi katika sekta hiyo umeonyesha matunda yanayoleta manufaa kwa nchi na Watanzania kwa ujumla.

**(Lilian Lucas)**

### Anusurika kifo kwa kugonga wanyama hifadhini Mikumi



**Morogoro.** Mfanyabiashara Thobias Mbilinyi (47), mkazi wa Makambako amenusurika kifo baada ya kugonga nyati wawili madume katika hifadhi ya Taifa ya Mikumi mkoani Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo Januari 10.

"Mwendo kasi ndio chanzo cha ajali, katika hifadhi kuna mwendo wake ambapo mchana ni kilomita 70 kwa saa na usiku ni kilomita 50 kwa saa, hakufuata taratibu hizo," alisema.

Mganga Mkuu mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Morogoro, Dk Daniel Nkungu alisema: "Nimempokea majeruhi huyo akitokea Hospitali ya Mtakatifu Kizito, ameumia usoni na shingoni, alipewa huduma ya dharura hapa na kusafirishwa kwenda Muhimbili".

**(Lilian Lucas)**

Scanned with CamScanner

mradi
ati

zi

i
li

a

li

## MAJADILIANO



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba (katikati) akijadiliana jambo na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kushoto) na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega baada ya kuhitimisha kikao kwa njia ya mtandao na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (Badea), Dk Sidi Ould Tah, jijini Dodoma juzi. **Picha na WFM**

Scanned with CamScanner